Ripoti ya Uwajibikaji

Viashiria vya Rushwa, Ubadhirifu na Udanganyifu Katika Taasisi za Umma

2020/21

Ripoti ya Uwajibikaji

Viashiria vya Rushwa, Ubadhirifu na Udanganyifu Katika Taasisi za Umma

2020/21

Co-funded by European Union

german cooperation
DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Embassy of Switzerland in Tanzania

giz Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH

Embassy of Sweden
Dar es Salaam

ROYAL NORWEGIAN EMBASSY

Yaliyomo

UTANGULIZI ..... **ii**

Maana ya Viashiria vya Rushwa, Udanganyifu na Ubadhirifu 1

Vigezo Vilivyotumika Kubainisha Viashiria vya Rushwa, Udanganyifu na Ubadhirifu 3

VIASHIRIA VYA RUSHWA, UDANGANYIFU NA UBADHIRIFU 4

Jambo la 1: Upotevu wa Mapato ya Umma Shillingi 1,838.86 bilioni 5

Jambo la 2: Matumizi Yasiyo na Tija Shilling 1,140.39 bilioni Katika Usimamizi wa Matumizi ya Kawaida, Mishahara, Mafao na Rasilimaliwatu 8

Jambo la 3: Matumizi ya Shillingi 1,611.48 bilioni Katika Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba Yaliyo na viashiria vya Rushwa, Ubadhirifu na Udanganyifu 11

HITIMISHO: **16**

Utangulizi

Ripoti ya Uwajibikaji ya Viashiria vya Rushwa, Ubadhirifu na Udanganyifu katika taasisi za Umma imeandaliwa kutokana na ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Mamlaka ya Serikali za Mitaa za mwaka 2020/21. Dhumuni la ripoti hii ni kuzirahisisha ripoti za CAG ili kuwawezesha wadau wa uwajibikaji (kama vile AZAKI, Wawakilishi wa Wananchi, Taasisi za Elimu ya Juu na Vyombo vya Habari) kudai uwajibikaji hapa nchini.

WAJIBU inatambua kuwa dhana ya mapambano dhidi ya rushwa siyo ya TAKUKURU pekee, ndiyo maana WAJIBU imeona ina wajibu na jukumu kama AZAKI kutoa taarifa hizi za viashiria vya rushwa, ili kuchochea mapambano dhidi ya rushwa. Pia, WAJIBU inazishauri mamlaka husika kuanza kufanya uchunguzi kuhusu viashiria hivi vya rushwa na kuchukua hatua stahiki kwa wahusika ili kukomesha vitendo vya rushwa nchini. WAJIBU inatarajia ripoti hii itawakumbusha watendaji wa Serikali umuhimu wa kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na CAG kuhusu vitendo vinavyoashiria rushwa, ubadhirifu na udanganyifu katika ukusanyaji na utumiaji wa fedha na rasilimali nyingine za umma. Vilevile, ripoti hii itawawezesha wananchi kuelewa namna rasilimali za Umma zilivyotumika katika kuwaletea maendeleo.

Ripoti hii imejikita katika kuelezea maana ya viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu; kuchambua maeneo yenye viashiria vya rushwa; udanganyifu na ubadhirifu; utoaji wa mapendekezo ya WAJIBU katika kupambana na rushwa, ubadhirifu na udanganyifu.

WAJIBU inawakaribisha wananchi na wadau wengine wote kuisoma ripoti hii na kutoa maoni yatakayochangia kuboresha uwajibikaji wa taasisi za umma na serikali kwa ujumla.

Maana ya Viashiria vya Rushwa, Udanganyifu na Ubadhirifu

Kwa mujibu wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wa Awamu ya Tatu 2017-2022 (NASCAP III), vitendo vya rushwa vinatafsiriwa kuwa ni kutoa, kupokea kitu chochote cha thamani, kushawishi moja kwa moja au vinginevyo ili kupindisha utaratibu katika utoaji wa maamuzi.

Rushwa ni janga ambalo lina athari hasi katika jamii. Athari hizo ni pamoja na kudhoofisha ustawi wa demokrasia katika nchi; ukiukwaji wa haki za binadamu; kuharibu mfumo wa masoko; kusababisha mmomonyoko wa maadili katika jamii; kuchelewesha maendeleo ya nchi; kuruhusu uhalifu wa kupangwa, ugaidi na vitisho vingine kwa usalama wa Taifa. Athari nyingine ni kuumiza wananchi kwa kuchepusha rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa matumizi na manufaa ya watu wachache, kudhoofisha uwezo wa Serikali wa kutoa huduma za msingi, kukosekana kwa usawa na haki na kukatisha tamaa wananchi kulipa kodi na kukatisha tamaa wafadhili (wadau wa maendeleo) na wawekezaji kuendelea kuchangia maendeleo ya nchi.

Kwa njia moja au nyingine, rushwa uhusiana na udanganyifu ambao unahusisha kutotimiza wajibu, kujitambulisha kwa uongo au jaribio la kupotosha ukweli ili kujinufaisha kifedha au kwa namna nyingine yeyote. Kwa hiyo, rushwa na udanganyifu huathiri maendeleo ya uchumi wa nchi na ni adui mkubwa katika utoaji wa haki, kupunguza umaskini na kukuza uchumi. Rushwa, udanganyifu na ubadhirifu ni vitendo vinavyopelekea ufisadi. Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi ISA 240, ISSAI 1224 pamoja na ISSAI 1315 vinatoa maana ya udanganyifu au ufisadi kuwa ni " kitendo au vitendo vya makusudi kinacho(vinavyo)fanywa na watu au mtu kwa ajili kunufaika kwa njia haramu au isiyo ya haki".

Mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi ni suala muhimu kwa kuwa athari zake ni kubwa katika harakati za kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Endapo suala la rushwa litaendelea kutokuchukuliwa hatua stahiki, juhudi za kujenga uchumi imara ambao utachangia kupunguza kiwango cha umasikini wa wananchi hazitoweza kuzaa matunda tarajiwa.

Ripoti ya Tume ya Rais ya Kupunguza Kero za Rushwa[1], ilibainisha namna rushwa inavyoweza kujidhihirisha kupitia njia kuu mbili ambazo ni:

(a) Rushwa katika Mifumo ya Utawala

Hii inatokana na watumishi wa Serikali na mawakala wao kudai rushwa wakati wa kutoa huduma za bure kwa wananchi. Taarifa hiyo imeeleza kuwa aina hiyo ya rushwa uchwara inasababishwa na viwango vidogo vya mishahara vinavyolipwa kwa wafanyakazi ambavyo havikidhi mahitaji yao.

1 Ripoti ya Tume ya Rais ya Kupunguza Kero za Rushwa ya mwaka 1996,



(b) Rushwa Kabambe (Kubwa)

Aina hii ya rushwa imebainishwa kuhusisha Viongozi wa Ngazi za juu Serikalini, wenye Mamlaka ya kutoa maamuzi kupitia Sera na mikataba. Taarifa hiyo imebainisha kuwa, sababu kubwa ya rushwa hiyo ni ulafi uliokithiri wa kujilimbikizia mali kwa watumishi wa serikali wasiowaaminifu katika utendaji wa kazi zao.

Hata hivyo, taarifa ya hali ya mtazamo wa jamii kuhusu rushwa inayotolewa na shirika la kimataifa katika masuala ya uwazi ya mwaka 2021 (Corruption Perceptions Index of Transparency International), imeonesha kuwa Serikali ya Tanzania imepata alama 39 kati ya 100 katika mapambano dhidi ya adui rushwa[2]. Utafiti huo ulionesha kuwa Tanzania imeshika nafasi ya 87 kati ya nchi 180 katika mapambano dhidi ya rushwa ulimwenguni. Hali hii inaonesha kuwa, bado jitihada kubwa za mashirikiano zinahitajika kufanywa na wadau wote katika mapambano dhidi ya rushwa.

2 https://www.transparency.org/en/cpi/2021/index/tza



Vigezo Vilivyotumika Kubainisha Viashiria vya Rushwa, Udanganyifu na Ubadhirifu.

Katika uchambuzi wa ripoti za CAG, yapo maeneo ambayo yanaonesha uwepo wa viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu. WAJIBU imetumia vigezo vifuatavyo katika kuainisha maeneo hayo:

a) Mapato kutopelekwa benki,
b) Kukosekana kwa hati za malipo,
c) Kutumia hundi za malipo zilizoghushiwa,
d) Kufanya malipo kinyume na matakwa ya Sheria, Kanuni na Taratibu za manunuzi,
e) Kupokea huduma au bidhaa kwa uthibitisho wa uongo,
f) Malipo ya huduma au bidhaa ambazo hazijatolewa au hazijapokelewa,
g) Malipo kwa watumishi hewa,
h) Matumizi mabaya ya nafasi au cheo,
i) Malipo kwa makandarasi ambao hawajulikani (wakandarasi hewa),
j) Kupokea huduma au bidhaa zisizo sahihi au ambazo hazikidhi mahitaji,
k) Kupokea huduma au bidhaa mbadala bila makubaliano halali, na
l) Makusanyo ya fedha za umma yaliyofanyika nje ya mfumo wa GePG.

Kwa kutumia vigezo vilivyoainishwa hapo juu, ripoti za CAG za mwaka 2020/21, zinaonesha kuwepo kwa matukio mbalimbali yanayoashiria rushwa, udanganyifu na ubadhirifu wa fedha na rasilimani za umma kama yalivyochambuliwa katika ripoti hii.

VIASHIRIA VYA RUSHWA, UDANGANYIFU NA UBADHIRIFU

Katika uchambuzi wa ripoti za CAG za mwaka 2020/21, WAJIBU imeainisha maeneo yenye viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu wa fedha za umma. Kwa sababu mbalimbali zinazoashiria vitendo vya rushwa, Serikali imeshindwa kukusanya mapato yaliyoainishwa kwenye bajeti na kufanya matumizi mabaya yasiyo na tija kisera na kijamii. Kiasi ambacho aidha hakikukusanywa au kimetumika na Serikali pasipo kupata tija yoyote (nugatory expenditure) kimekua kwa asilimia 159 kutoka Shilingi 1,770.84 bilioni mwaka 2019/20 hadi kufikia Shilingi 4,590.73 bilioni mwaka 2020/21. Hii ni sawa na asilimia 15 ya fedha zote zilizotumika katika mwaka wa fedha 2020/21 zilizofikia Shilingi 31,373.19 bilioni.

Serikali Kuu ndiyo imekua na ongezeko kubwa zaidi la asilimia 218 kutoka Shilingi 560.19 bilioni mwaka 2019/20 hadi Shilingi 1,781.77 bilioni kwa mwaka 2020/21. Viashiria vya rushwa katika Serikali Kuu pekee vya Shilingi 1,781.77 bilioni ni sawa na asilimia 38.81 ya jumla yote ya viashiria vya rushwa vya Shilingi 4,590.73 bilioni kwa mwaka 2020/21, ambapo kasoro nyingi zilionekana katika eneo la ununuzi wa umma na mapungufu ya usimamizi wa kina wa mikataba, kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 1.

Jedwali Na. 1: Mwenendo wa Viashiria vya Rushwa, Ubadhirifu na Udanganyifu kwa kipindi cha Miaka Mitatu (2018/19 – 2020/21).

	2018/19	2019/20	2020/21
	SHILINGI Bilioni		
Jumla	*232.52*	*1,770.84*	4,590.73
Serikali Kuu	*34.3*	*560.19*	*1,781.77*
Mamlaka za Serikali za Mitaa	*103.93*	*863.85*	1,400.60
Mashirika ya Umma	*94.29*	*346.80*	1,408.36

Jumla ya viashiria vyote vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu vya Shilingi 4,590.73 bilioni vilikua ni asilimia 15 ya matumizi yote ya Serikali ya Shilingi 31,373.19 billioni mwaka 2020/21. Viashiria vya vitendo vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu vinaoneshwa katika jedwali Na.2 na maelezo yanayofuata.

Jedwali Na 2: Mchanganuo wa maeneo ambayo yana viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu katika Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma kwa mwaka 2020/21

	Serikali Kuu	Serikali za Mitaa	Mashirika ya Umma	Jumla
	Shilingi Bilioni			
Jambo la 1: Upotevu wa Mapato ya Fedha za Umma Shilingi 1,838.86 Bilioni	1,050.02	293.31	495.53	1,838.86
Jambo la 2: Matumizi yasiyo na tija Shilingi 1,140.39 bilioni katika Usimamizi wa Mishahara, Mafao na Rasilimali watu.	53.9	1,066.38	20.11	1,140.39
Jambo la 3: Matumizi ya Shilingi 1,611.48 bilioni katika Manunuzi na Mikataba yanayoashiria vitendo vya Rushwa, Ubadhirifu na Udanganyifu.	677.85	40.91	892.72	1,611.48
	1,781.77	1,400.6	1,408.36	4,590.73

Jambo la 1: Upotevu wa Mapato ya Umma Shilingi 1,838.86 bilioni

Kutokana na udhaifu katika mifumo ya ukusanyaji wa mapato, Serikali inaweza kuwa imepoteza Shilingi 1,838.86 bilioni kwa sababu ya vitendo vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu. Kiasi kikubwa cha fedha hizi kinatokana na kasoro zilizojitokeza katika ukusanyaji wa mapato katika Serikali Kuu kama inavyoonekana katika Jedwali Na 3.

Jedwali Na 3: Mchanganuo wa kiasi ambacho kina viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu katika ukusanyaji wa mapato katika Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma

UPOTEVU WA MAPATO KIASI CHA SHILLINGI 1,838.86 bilioni							
Mwaka	Serikali za Mitaa		Serikali Kuu		Mashirika ya Umma		Jumla
	Shilingi Bilioni	%	Shilingi Bilioni	%	Shilingi Bilioni	%	Shilingi Bilioni
2018/19	44.03	85%	7.7	15%	-		51.73
2019/20	191.2	72%	38.7	15%	35.96	14%	265.86
2020/21	293.31	16%	1,050.02	57%	495.53	27%	1,838.86

Serikali Kuu:

Baadhi ya mapungufu yaliyopelekea upotevu wa Shilingi 1,050.02 bilioni, katika ukusanyaji wa mapato ya ndani katika Serikali Kuu ni kama yafuatayo:

a. Malipo ya ndege na abiria kwa kutumia uwanja wa ndege Arusha (Airport Departure Charges) yaliyokusanywa na KADCO hayakupelekwa Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) kiasi cha Shilingi 2.37 bilioni na Dola za Kimarekani 7.04 milioni sawa na Shilingi 16.17 bilioni.
b. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), haikukusanya tozo ya Shilingi 13.40 bilioni, kutoka kwa makampuni yaliyosababisha mabadiliko katika mfumo wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja. Kampuni hizo bado zilikuwa zikiendelea kushiriki katika michakato ya ununuzi wakati zikiwa hazistahili kwa kuwa zilikuwa zimefungiwa kushiriki.
c. Makusanyo yaliyofanyika nje ya mfumo wa GePG Shilingi 6.53 bilioni. Pia, Idara ya Uchapaji ya Serikali na Mamlaka mbili za Maji zilishindwa kukusanya makusanyo ya Shilingi 8.8 bilioni kutokana na kutokuwa na uwezo wa kutoa huduma.

Serikali za Mitaa:

Baadhi ya mapungufu yaliyopelekea upotevu wa Shilingi 293.31 bilioni, katika ukusanyaji wa mapato ya ndani katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni kama ifuatavyo:

a. Mamlaka za Serikali za Mitaa 94 hazikukusanya mapato ya leseni za biashara kiasi cha shilingi 9.01 bilioni. Pia, Halmashauri 14 zilitoa leseni za Shilingi 1.93 billioni wakati fedha zilizokusanywa kutokana na utoaji wa leseni hizo ni shilingi 2.64 bilioni, ikimaanisha kuwa malipo ya Shilingi 718.28 millioni hayakukusanywa au kama yalikusanywa basi hayakuwasilishwa kwenye Halmashauri husika.
b. Halmashauri ya Manispaa ya Temeke haikukusanya Ushuru wa Huduma wa Shilingi 1.92 billioni kutokana na ukosefu wa mfumo wa kielektroniki wa kupeana taarifa za mauzo ghafi kati ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na TRA. Pia, Halmashauri 43 zilikusanya ushuru wa huduma wenye jumla ya Shilingi 9.01 billioni bila kupata ushahidi wa taarifa za mauzo ghafi kutoka mamlaka husika au taasisi husika ili kuthibitisha usahihi wa kiasi kilichokusanywa.
c. Mamlaka 27 za Serikali za Mitaa zilirekebisha ankara za kiasi cha Shilingi 1.66 billioni katika Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato bila maelezo na/au viambatisho toshelevu ili kuhalalisha mabadiliko ya ankara zinazohusika wakati baadhi ya Halmashauri zilifanya marekebisho bila idhini ya Wakurugenzi wao.

d. Wakusanya mapato kupitia POS katika mamlaka 147 za Serikali za Mitaa hawakuwasilisha jumla ya Shilingi 17.0 billioni katika akaunti za benki za Halmashauri husika. Hii inatokana na kutofanyika kwa usuluhishi wa mara kwa mara wa hesabu (angalau kwa wiki) na kukosekana kwa ufuatiliaji wa karibu wa makusanyo ya Halmashauri ili kuhakikisha makusanyo ya mapato yanawekwa benki kwa wakati.

Mashirika ya Umma:

Katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Mashirika ya Umma, baadhi ya mapungufu yaliyopelekea upotevu wa Shilingi 495.53 bilioni ni kama ifuatavyo:

a. Shirika la Umeme (TANESCO) lilipata hasara ya Shilingi 105.49 billioni kutokana na punguzo za tozo za mauzo ya nishati na uunganishaji wa huduma za umeme; pia rakili za mita (meter seal) 5,000 za Shirika ziligunduliwa katika duka la mtaani, hali iliyoashiria upotevu wa mapato kutokana na wizi wa rakili hizo za mita.

b. Wateja 375 wa Shirika la Bima la Taifa, hawakulipa fedha za tahadhari zenye jumla ya Shilingi 220.11 milioni. Hata hivyo, CAG alibaini kuwa wateja hao hawakulipa fedha hizo kutokana na ukaidi.

c. Mapato yenye thamani ya Shilingi 2.22 bilioni yalikusanywa nje ya mfumo wa kielekitroniki wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali (GePG).

Jambo la 2: Matumizi Yasiyo na Tija Shilingi 1,140.39 bilioni katika usimamizi wa Matumizi ya Kawaida, Mishahara, Mafao na Rasilimaliwatu

CAG ameonesha, kuna viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu katika matumizi ya Shilingi 1,140.39 bilioni kwa mwaka 2020/21 kutokana na kasoro za usimamizi wa matumizi ya kawaida, mishahara, mafao na rasilimaliwatu. Kiasi hiki kimeongezeka kwa Shilingi 759.47 bilioni kutoka Shilingi 380.92 bilioni cha mwaka 2019/20. Katika matumizi ya kawaida, mishahara, mafao na rasilimaliwatu ambayo yanaviashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu, Mamlaka ya Serikali za Mitaa zilikuwa na kiasi kikubwa zaidi cha Shillingi 1,066.38 bilioni zikifuatiwa na Serikali Kuu Shilingi 53.9 bilioni na Mashirika ya Umma Shilingi 20.11 bilioni kama inavyoonekana katika jedwali Na 5.

Jedwali Na.5: Mchanganuo wa kiasi ambacho kina viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu katika Matumizi ya kawaida, mishahara, mafao na rasilimaliwatu katika Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma

MATUMIZI YASIYO NA TIJA KATIKA USIMAMIZI WA MATUMIZI YA KAWAIDA, MISHAHARA, MAFAO NA RASILIMALIWATU							
Mwaka	Serikali za Mitaa		Serikali Kuu		Mashirika ya Umma		Jumla
	Shilingi Bilioni	%	Shilingi Bilioni	%	Shilingi Bilioni	%	Shilingi Bilioni
2018/19	0.64	4%	0.2	1%	13.75	94%	14.59
2019/20	82.21	22%	104.6	27%	194.11	51%	380.92
2020/21	1,066.38	93%	53.9	5%	20.11	2%	1,140.39

Serikali Kuu:

Baadhi ya maeneo yaliyokuwa na viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu katika Serikali Kuu, ni kama ifuatavyo:

a. Katika eneo la usimamizi wa matumizi, taasisi 48 kwenye Serikali Kuu zilifanya matumizi ya Shilingi 6.35 bilioni bila ya kuwa na nyaraka stahiki na toshelezi; taasisi nane zilifanya malipo yasiyo na tija ya Shilingi 482.59 milioni; na taasisi 24 zilifanya malipo ya Shilingi 4.57 bilioni kwenye vifungu visivyohusika. Pia, kulikuwa na taasisi 19 zilizofanya malipo ya Shilingi 6.17 bilioni zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa bila kuwa na uthibitisho wa vibali cha kubadili matumizi; Taasisi 30 zilikuwa na masurufu ambayo hayajarejeshwa ya Shilingi 3.42 bilioni; na taasisi nane zilitumia masurufu ya Shilingi 823.49 milioni kama matumizi kinyume na Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (kama zilivyorekebishwa).

b. Katika ukaguzi wa rasilimaliwatu na malipo ya mishahara, kama ilivyokuwa katika miaka iliyopita, CAG alibaini taasisi za Serikali ambazo hazikuwasilisha makato ya kisheria kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Taasisi nyingine ya kiasi cha Shilingi. 391.68 milioni, pamoja na malipo ya mishahara bila mikataba ya ajira yenye thamani ya Shilingi 348.49 milioni.
c. Wizara ya Kilimo ilitekeleza Mradi wa Kuongeza Uzalishaji wa Mpunga (ERPP) wenye lengo la kuongeza tija na uzalishaji wa mpunga mkoa wa Morogoro. Mradi huu ulifadhiliwa na Mfuko wa Dhamana wa Mpango wa Kilimo na Usalama wa Chakula Duniani (GAFSP) na kusimamiwa na Benki ya Dunia. Wizara ya Kilimo ilifungua akaunti ya mradi katika Benki Kuu ya Tanzania. Benki Kuu ya Tanzania ilihamisha kiasi cha Dola za Marekani 298,500 ambazo ni sawa na Shilingi 666.12 milioni kutoka kwenye akaunti ya mradi wa ERPP kwenda kwenye Kampuni ya Rich Host Enterprises Group Limited kwa njia ya udanganyifu kwa kutumia barua ya kuhamisha fedha iliyoghushiwa.

Mamlaka ya Serikali za Mitaa:

Baadhi ya maeneo yaliyokuwa na viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ni kama ifuatavyo:

a. CAG alibaini kuwa Halmashauri 25 zililipwa kutoka Hazina jumla ya Shilingi 556.84 milioni kwa watumishi ambao hawakuwepo kazini kwa mfano watumishi wastaafu, waliofariki, watoro, walioachishwa kazi na waliopewa likizo bila malipo.
b. CAG alibaini, makato ya kisheria yenye thamani ya shilingi 845.24 milioni hayakupelekwa katika taasisi husika, hivyo kusababisha deni la shilingi 180.70 bilioni linalotokana na adhabu zilizotolewa kwa Halmashauri tano kwa kushindwa kuwasilisha makato ya kisheria.
c. CAG alibaini kuwa mamlaka 24 za Serikali za Mitaa zilitumia shilingi 664 milioni kwenye matumizi yasiyo na manufaa. Pia, Mamlaka 61 za Serikali za Mitaa ziliagiza na kulipa shilingi 8.44 bilioni kwa ajili ya bidhaa/huduma ambazo hazikupokelewa toka kwa wazabuni kwa muda wa hadi kufikia miezi 24; na mamlaka 64 za Serikali za Mitaa hazikuwa na hati za malipo na viambatisho vya matumizi ya thamani ya Shilingi 3.87 bilioni.

Mashirika ya Umma:

Baadhi ya maeneo yaliyokuwa na viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu katika Mashirika ya Umma, ni kama ifuatavyo:

a. Mashirika na taasisi zingine za umma nne katika mwaka 2020/21 hazikupeleka michango ya kisheria ya Shilingi 129.33 bilioni kwenye mifuko ya pensheni, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi.
b. Mashirika sita ya umma yalifanya miamala ya malipo katika shughuli mbalimbali yenye thamani ya Shilingi 4.42 bilioni, lakini malipo hayo hayakuwa na nyaraka sahihi za kuthibitisha uhalali wa gharama hizo.

c. Matumizi yasiyostahili yenye thamani ya Shilingi 897.89 millioni katika Mashirika na taasisi nyingine za umma

Jambo la 3: Matumizi ya Shilingi 1,611.48 bilioni Katika Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba Yanaviashiria vya Rushwa, Ubadhirifu na Udanganyifu

Kifungu cha 48 (3) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 kinamtaka CAG kueleza katika ripoti yake ya ukaguzi ya mwaka iwapo taasisi alizozikagua zimezingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake.

Katika ununuzi wa umma na usimamizi wa mikataba, kuna viashiria vya Shilingi 1,611.48 bilioni kuwa zimetumika bila kuwepo na tija kutokana na kuwa na dalili zote za kuwepo na vitendo vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu. Kumekuwepo na kiasi kikubwa cha matumizi katika ununuzi wa umma na usimamizi wa mikataba cha Shilingi 892.72 bilioni kwenye Mashirika ya Umma; Shilingi 677.85 bilioni kwenye Serikali Kuu na Shilingi 40.91 billioni kwenye Serikali za Mitaa ambayo yanaviashiria vya uwepo wa rushwa, udanganyifu na ubadhirifu wa fedha za umma kama inavyoonekana kwenye jedwali Na.6.

Jedwali Na. 6: Mchanganuo wa kiasi ambacho kina viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu katika Ununuzi wa Umma na Usimamizi wa Mikataba katika Serikali Kuu, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma

MANUNUZI NA MIKATABA YENYE VIASHIRIA VYA RUSHWA.							
Mwaka	**Serikali za Mitaa**		**Serikali Kuu**		**Mashirika ya Umma**		**Jumla**
	Shilingi Bilioni	**%**	**Shilingi Bilioni**	**%**	**Shilingi Bilioni**	**%**	**Shilingi Bilioni**
2018/19	59.26	36%	26.4	16%	80.54	48%	166.2
2019/20	590.44	53%	416.89	37%	116.74	10%	1,124.07
2020/21	40.91	3%	677.85	42%	892.72	55%	1,611.48

Serikali Kuu:

Baadhi ya kasoro zilizobainishwa na CAG zenye viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu ni pamoja na:

a. Shilingi 10.34 bilioni zilizopelekwa kwa Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) kwa ajili ya kununua magari lakini magari hayo hayajapokelewa na Wizara, Idara na Wakala 17.

b. Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) na Idara ya Jeshi la Magereza walikatisha mikataba mitatu yenye jumla ya Shilingi 126.55 bilioni pasipo kufuata taratibu za kusitisha mikataba, ikiwa ni pamoja na kutatua migogoro na kuomba ushauri wa kisheria kutoka kwa mamlaka husika ikiwemo Ofisi ya

Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kusitisha mikataba pasipo kufuata sheria kunaweza kuiingizia Serikali hasara endapo Wakandarasi wataamua kudai haki zao.

c. Ukaguzi maalumu juu ya tuhuma za ubadhirifu za noti chakavu zilizorejeshwa Benki Kuu ya Tanzania, ulibaini kuwa noti 399,392 zenye thamani ya Shilingi 3.99 bilioni hazikuwa zimekidhi vigezo vya kuwa noti chakavu na zilibadilishwa na kutolewa noti safi kwa njia ya udanganyifu na maofisa wawili na watunza fedha wanne wa Benki Kuu.

d. Kuanzia tarehe 16 hadi 22 Agosti 2021, TAWA ilifanya mnada wa kielektroniki kwenye vitalu mbalimbali vya uwindaji, ambapo makampuni 28 yalishiriki katika mnada huo, na makampuni sita (wazabuni wenye bei ya juu zaidi) walipewa vitalu vya uwindaji. Wazabuni hao walioshinda zabuni waliilipa Serikali kiasi cha Shilingi. 282.5 milioni, ikiwa ni asilimia 100 (25% na 75%) ya kiasi kilichotajwa kwa mujibu wa Kifungu cha 1.2 (iv & v) cha Mwongozo wa Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji kwa Njia ya Mnada, ambao uko chini ya Kifungu cha 38 cha Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori, Sura Na. 283. Hata hivyo, tarehe 04 Novemba 2021, Waziri (Wizara ya Maliasili na Utalii) alisitisha na kufuta mchakato mzima wa mnada wa kielektroniki kwa sababu ya kuwepo kwa malalamiko kadhaa yaliyowasilishwa dhidi ya mchakato huo, licha ya jitihada za TAWA kujibu malalamiko hayo kwa maelezo na ushahidi wa maandishi. Kwa maoni ya CAG, mnada huu wa kielektroniki ulifanywa kwa njia ya kielektroniki bila uingiliwaji wa aina yoyote kama ilivyobainishwa katika Sehemu ya 1.2 (iv & v) ya Mwongozo wa Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji kwa Njia ya Mnada ambao uko chini ya Kifungu cha 38 cha Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori, Sura Na. 283, hivyo kupunguza uwezekano wa upendeleo. Pamoja na hayo, Waziri angeweza kuchunguza mchakato mzima wa utendaji kazi wa mfumo kabla ya kufuta zabuni husika na kuisababishia Serikali malalamiko na gharama.

Mamlaka ya Serikali za Mitaa:

Katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, baadhi ya kasoro zilizobainishwa na zenye viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu ni pamoja na:

a. Mamlaka 24 za Serikali za Mitaa zilifanya ununuzi wenye thamani ya shilingi 3.84 bilioni bila kuzingatia mpango wa ununuzi wa kila Halmashauri husika.
b. Mamlaka 39 za Serikali za Mitaa zilifanya ununuzi wenye thamani ya Shilingi 5.37 bilioni bila kuitisha nukuu za bei za ushindani, ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze inaongoza kwa kufanya ununuzi wa Shilingi 1.73 bilioni.
c. Kiasi cha shilingi 310.42 milioni hakikurudishwa na wakandarasi baada ya kuvunjika kwa mikataba katika Halmashauri za Wilaya ya Madaba na Kibondo kama ifuatavyo:
    - Halmashauri za Wilaya ya Madaba na Kibondo hazikurejeshewa kiasi cha Shilingi 229.76 milioni na Shilingi 51.43 milioni mtawalia ikiwa ni asilimia 40 ya thamani ya kazi ambazo hazikufanyika kutoka kwa wakandarasi wawili hali iliyosababisha Halmashauri hizo kuingia gharama za ziada katika kumalizia kazi hizo.
    - Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo haikurudishiwa jumla ya Shilingi 29.23 milioni zilizohesabika kama gharama za uvunjaji wa mkataba ambazo zililipwa kwa mkandarasi kinyume na utaratibu wa mkataba.

Mashirika ya Umma:

Katika Mashirika ya Umma, baadhi ya kasoro zilizobainishwa na zenye viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu ni pamoja na:

a. Katika ukaguzi wa uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na miongozo katika michakato ya ununuzi wa ujenzi, CAG alibaini mashirika 79 hayakuzingatia sheria ya manunuzi. Mapungufu yaliyobainika ni pamoja na:
    - Maofisa Masuuli kuingilia majukumu ya bodi ya zabuni kwa kuidhinisha utoaji wa mikataba yenye thamani ya Dola za Marekani 1.06 milioni na Shilingi 2.79 bilioni;
    - Ununuzi ulifanyika bila mikataba halali yenye thamani ya Shilingi 9.90 bilioni na Dola za Marekani 1.42 milioni katika Bohari Kuu ya Dawa.
    - Mashirika 23 ya umma yalifanya ununuzi wa Shilingi 57.38 bilioni, Dola za Marekani 5.23 milioni na Euro 176,710 kwa zabuni 514 nje ya Mfumo wa Kielekitroniki wa Ununuzi wa Umma (TANePS).

b. Upanuzi wa Bandari ya Tanga: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari iliingia mkataba na "Mkandarasi Mkuu" wa Shilingi 172.36 bilioni tarehe 3 Agosti 2019 wa muda wa mwaka mmoja hadi kufikia mwezi Agosti 2020 kwa ajili ya kuongeza kina cha lango na sehemu ya kugeuzia meli katika bandari ya Tanga, kufanya tathmini ya athari za kimazingira, na kununua vifaa kwa ajili ya shughuli za bandari. Kwa kulingana na mkataba, gharama ya kuongeza kina cha lango na sehemu ya kugeuzia meli katika Bandari ya Tanga ilikuwa ni Shilingi 104.92 billioni (asilimia 60 ya bei yote ya mkataba). Katika ukaguzi wake CAG alibaini kuwa, mnamo tarehe 1 Agosti 2019, "Mkandarasi Mkuu" iliingia makubaliano na "Mkandarasi Mbia" kwa ajili ya kazi ya kuongeza kina

cha lango na sehemu ya kugeuzia Meli kwa bei ya mkataba wa Dola za Marekani 18.15 milioni sawa na Shilingi 40.46 bilioni kwa kipindi cha miezi 11. Cha ajabu ni kuwa:

- Mkandarasi Mkuu aliingia mkataba na Mkandarasi Mbia siku 2 kabla ya yeye kuwa na mkataba na pia hakutoa taarifa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari.
- Ukilinganisha bei ya mkataba kati ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari na Mkandarasi Mkuu pamoja na bei ya mkataba kati ya Mkandarasi Mkuu na Mkandarasi Mbia utabaini kuwa, Mkandarasi Mkuu alipata faida ya shilingi 64.46 bilioni pasipo kufanya kazi yoyote.

HITIMISHO:

Masuala yaliyochambuliwa katika ripoti hii yanalenga kutoa taarifa kwa wananchi na wadau mbalimbali juu ya uchambuzi wa ripoti za CAG za mwaka 2020/21. Katika ripoti hii, WAJIBU imeainisha maeneo 3 yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu ambayo yana umuhimu mkubwa kwa jamii kuhusu utendaji na uwajibikaji wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma.

Aidha, uchambuzi wa ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali za mwaka 2020/21 umeonesha ongezeko la asilimia 159 ya makusanyo na matumizi ambayo yanaviashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu katika taasisi za umma. Hali hii isipodhibitiwa inaleta athari kubwa katika jitihada za Serikali za utoaji wa huduma kwa wananchi na kuipunguzia Serikali mapato hivyo kuwaongezea wafanyabiashara mzigo wa kodi.

Serikali imekusanya mapato asilimia 10 chini ya mapato yaliyokadiriwa katika bajeti ya mwaka 2020/21. Utofauti huo umesababisha bajeti kutokuwa ya uhalisia ambapo viwango vya kimataifa vya uhalisia vya bajeti vinataka bajeti isizidi au isipungue asilimia 5 ya utofauti huo. Pamoja na sababu nyingi nyingine, tatizo hili limechangiwa na viashiria vya rushwa katika kukusanya mapato. Fedha zilizopotea kutokana na viashiria vya ubadhirifu na rushwa zingeweza kupunguza malipo ya mwaka 2020/21 ya deni la Taifa kwa kiwango cha asilimia 49.04 takribani nusu ya malipo hayo. Hii ingeiwezesha Serikali kufikia malengo yake ya kutoa huduma kwa wananchi na kuendelea kujenga miundombinu na mazingira endelevu ya kiuchumi na kijamii kama vile miradi ya elimu na afya.

USHAURI:

WAJIBU inaishauri Serikali, Vyombo vya habari, wabia wa maendeleo pamoja na taasisi za kiraia kufanya mambo yafuatayo;

- Serikali kuiwezesha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani (IAG) kuwa na fungu lake (Vote) ili kumuongezea uwezo wa kufanya kazi zake kwa uhuru zaidi. Aidha, WAJIBU inashauri Mkaguzi Mkuu wa Ndani awe anapeleka taarifa hizi za mwaka kwa Katibu Mkuu Kiongozi Ikulu, ili taarifa zake zifikishwe kwenye Baraza la Mawaziri ambalo Rais wa Jamhuri ya Muungano ni Mwenyekiti wake. Ripoti hiyo imfikie Rais kabla ya tarehe 30 Septemba ambapo itakua ni miezi 9 baada ya mwaka wa fedha wa Serikali kumalizika. Hii itampa fursa Rais ya kujua hali au utendaji wa Serikali yake na inapolazimika kuanza kuchukua hatua kabla ya taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoka.

- Serikali kupitia **Ofisi ya Rais**, Menejimenti **ya Utumishi** wa Umma na Utawala Bora kuielekeza TAKUKURU kuifanya Ripoti Yake ya Utendaji ya Mwaka inayowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais sambamba na Ripoti za CAG kuwa ripoti ya wazi kwa umma. Hii itaboresha na kurahisisha utoaji na upokeaji wa taarifa za rushwa kutoka TAKUKURU na serikali kwa ujumla. Pia, itazidi kujenga imani ya wananchi kwa Serikali kwa kuonesha kuchukua hatua pale ambapo rushwa inahusishwa na utendaji hafifu wa

Serikali katika kukusanya mapato na katika matumizi mabaya ya fedha za umma. Vita dhidi ya rushwa inahusu wananchi wote, hivyo hakuna sababu ya kuwepo usiri katika mapambano hayo.

- Vyombo vya Habari viendelee kutumia fursa ya ripoti za uwajibikaji zilizorahisishwa kutoka katika ripoti za CAG, kuuhabarisha umma pamoja na kufuatilia masuala mbalimbali ya uwajibikaji yaliyoibuliwa katika ripoti hizo. Hii itasaidia umma kushiriki katika mapambano ya vitendo vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu vinavyofanywa katika makusanyo na matumizi ya fedha za umma.

- Katika Ripoti za CAG, yapo maeneo ambayo vitendo vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu vimethibishwa na CAG kwa mfano. Mkataba wa upanuzi wa Bandari ya Tanga, kuchakata noti chakavu na utoaji wa fedha katika akaunti ya Wizara ya kilimo iliyo Benki Kuu kwa barua ya kughushi. WAJIBU inasisitiza, Serikali ichukuwe hatua kali za kinidhamu ikiwemo kuvitaka vyombo vyake vya uchunguzi kufikisha wahusika hao katika vyombo vya sheria.

WAJIBU - INSTITUTE OF PUBLIC ACCOUNTABILITY
S.L.P 13486,
Barabara ya Rose Garden Mtaa wa Ndovu, Nyumba No.10, Dar es Salaam
Baruapepe: wajibu.institute@gmail.com

WAJIBU_INSTITUTE

www.wajibu.or.tz